

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**



*Dar es Salaam
20 Aprili, 2026*

Barua pepe: press@ikulu.go.tz

**TAARIFA KWA UMMA
RAIS SAMIA AKUTANA NA UJUMBE WA MTANDAO WA VIONGOZI
WANAWAKE AFRIKA (AFLN)**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo amepokea ujumbe kutoka Mtandao wa Viongozi Wanawake Afrika (AFLN), Ikulu jijini Dar es Salaam.

Ujumbe huo, ulioundwa na Marais wastaafu na viongozi wanawake waandamizi kutoka Afrika na taasisi za kimataifa, akiwemo Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Liberia, Mhe. Ellen Johnson Sirleaf; Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Shirikisho la Kidemokrasia la Ethiopia, Mheshimiwa Sahle-Work Zewde; pamoja na Bi. Joyce Mends-Cole na Bi. Hawine Amdissa, umeipongeza Tanzania kwa kurejesha hali ya amani na utulivu kufuatia matukio ya vurugu ya wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, na kupongeza juhudi za Serikali katika kulinda umoja wa kitaifa na kurejesha shughuli za kawaida za kiuchumi na kijamii.

Viongozi hao wamesema Tanzania imeendelea kujijengea sifa ya kuwa nchi ya amani na utulivu barani Afrika, wakipongeza uongozi thabiti wa Rais Dkt. Samia katika kuiongoza nchi katika kipindi kigumu bila kuyumbisha utendaji wa taasisi na utulivu wa ndani.

Katika mazungumzo, ujumbe wa AFLN umeelekeza msisitizo katika umuhimu wa kuendeleza mageuzi ya kisiasa na kiutawala ili kuimarisha demokrasia, uwajibikaji na ushirikishwaji wa wadau. Pia umehimiza kukuza nafasi za uongozi kwa wanawake na kuimarisha ushiriki wao katika ngazi mbalimbali za maamuzi.

Ujumbe huo pia umeeleza utayari wake wa kuisaidia Tanzania kulea kizazi kipya cha viongozi wanawake, ukisisitiza umuhimu wa kuweka mifumo itakayowawezesha si tu kufika kwenye nafasi za uongozi, bali pia kuzitumikia vizuri nafasi hizo.



Rais Dkt. Samia ameushukuru ujumbe huo kwa ziara hiyo, akisisitiza dhamira ya Serikali ya kuendelea kulinda amani, kuimarisha umoja na mshikamano wa kitaifa, pamoja na kusukuma mbele mageuzi ya taasisi na utawala bora.

Amesema Tanzania itaendelea kupanua fursa za uongozi kwa wanawake na vijana, huku ikiendelea kushikilia misingi ya demokrasia, ushirikishwaji na maendeleo endelevu, na kuongeza kuwa nchi itaendelea kuimarisha ushirikiano na wadau katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Mkutano huo ni sehemu ya mawasiliano endelevu kati ya Serikali na washirika wa kimkakati, kwa lengo la kuimarisha nafasi ya Tanzania kama taifa lenye utulivu na linalotekeleza mageuzi.

TAARIFA KWA MHARIRI

African Female Leaders Network ni jukwaa linalowaunganisha viongozi wanawake wa sasa na wastaafu wa bara la Afrika kwa lengo la kuendeleza uongozi wa wanawake, ujenzi wa amani na utawala bora barani Afrika.



Bakari S. Machumu

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu